# Uwezeshwaji wa Kiswahili kama

# Wenzo wa Maarifa


**WAHARIRI**

John M. Kobia
Mosol Kandagor
Leonard Chacha Mwita
Joseph Nyehita Maitaria
Sheila P. Wandera-Simwa

# UWEZESHWAJI WA KISWAHILI KAMA WENZO WA MAARIFA

**WAHARIRI**
John M. Kobia
Mosol Kandagor
Leonard Chacha Mwita
Joseph Nyehita Maitaria
Sheila P. Wandera-Simwa

MOI UNIVERSITY PRESS

Moi University Press, Moi University, Eldoret

© Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi

Kimechapishwa 2019

ISBN: 978-9966-133-56-4

Kimetoleshwa na:
Utafiti Foundation
Outspan, Off Eldoret-Nakuru Road.
P. O. Box 884 – 30100, Eldoret, Kenya.
Tel: +254 722 313 515
Website: www.utafitifoundation.com

# SURA YA ISHIRINI NA MBILI

## Athari za Uandishi na Uchapishaji wa Vitabu vya Kiada katika Ufundishaji wa Kiswahili Nchini Kenya

Abai Rose Ajuma[1] na Carren Nyandiba[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Kibabii*
[2]*Chuo Kikuu cha Rongo*

**gulizi**

lishi ni mfanyiko ambao unahusiana na utungaji wa vitabu vya kiada na ziada, magazeti, gaji mashairi, magazeti na kadhalika. Kwa hivyo, uandishi katika lugha yoyote ile gemea kuwepo kwa watunzi wa miswada katika maeneo haya yote ili miswada hiyo iwe uchapishaji. Kwa upande mwingine katika mtazamo finyu, uchapishaji ni mfanyiko gamano kwani unahusu kuifanya miswada ya watunzi iwe vitabu, majarida, magazeti na alika. Aidha, uchapishaji pia unawajumuisha waandishi, wachapishaji, wauzaji vitabu na tubu (Ogechi, 2004).

a mgongo wa uchapishaji nchini Kenya ni vitabu vya kiada. Kila kampuni ingependa pisha na kuuza vitabu hivi. Lakini tangu uhuru Taasisi ya Elimu Kenya ilikuwa inaandaa ada ya vitabu vya kiada ambavyo vilishapishwa na Kenya Literature Bureau na Jomo atta Foundation. Serikali pia iliunda Kenya School Equipment Scheme ili ivinunue vitabu visambaza kwa skuli zote nchini. Kwa hivyo, si wachapishaji wa kibinafsi wala wauzaji wa fsi walifaidi kutoka kwa sekta hii. Sera hii iliendelea hadi 1999 ambapo Wizara ya Elimu mwongozo mpya. TEK ilikoma kuandaa miswada. Kila kampuni ya uchapishaji ingeandaa ambavyo vingechunguzwa na TEK na orodha ikapendekezwa. Somo moja lingeweza na orodha ya vitabu kadhaa vilivyopendekezwa. Kisha kamati za skuli zingeweza kuteua vya kununua kutokana na orodha hiyo. Kamati ziliwajumuisha walimu wa skuli na hama wawili wa halmashauri ya wazazi. Hatua hii iling'oa ukiritimba wa serikali.

iyo ilisababisha kuwepo kwa vitabu vya kiada tofauti vilivyoandikiwa na kuchapishwa itindo tofauti. Baadhi ya walimu nchini walitegemea sana kitabu cha kiada kimoja bila lea vitabu vingine kutokana na matini yaliyopatikana katika kitabu husika. Aidha, uteuzi nuzi wa vitabu vya kiada uliachiwa halmashauri ya shule na walimu wa madarasa nbali katika shule. Imebainika kuwa wakati mwingine kitabu cha kiada huteuliwa bila nu wa mwalimu husika. Pia, kuwepo kwa anwani nyingi tofauti za vitabu vya kiada akanganya walimu kwa sababu ya uhitilafiano kuhusu namna dhana na mambo oshughulikiwa na waandishi tofauti (Ipara, 2007).

i inadahili na kudadavua athari hasi na chanya za uandishi na uchapishaji wa vitabu vya ina aina katika ufundishaji wa Kiswahili. Aidha, sura inapendekeza hatua zinazoweza uliwa kuimarisha uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada vya Kiswahili kwa mujibu mo wa elimu katika shule za msingi na za upili nchini Kenya.

**Sera za Elimu**

Tangu Kenya ipate uhuru mwaka wa 1963 kumekuwepo na mageuzi si ya kisiasa tu bali pia kiuchumi na kiutamaduni. Utamaduni umejumuisha mambo mengi, elimu ikiwa ni mojawapo wa mambo hayo. Katika kipindi cha miongo mitano, mabadiliko mengi yametokea katika elimu. Mabadiliko hayo hasa yamejikita katika uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada. Altbach (1999) anadai kuwa skuli pamoja na Taasisi za Elimu ya juu, hutegemea vitabu na machapisho mengine ili kuyatimiza malengo ya kielimu kati ya uchapishaji na mfumo wa elimu katika viwango vyote.

Kwa sasa nchini Kenya hakuna sera madhubuti ya uandishi na uchapishaji wa vitabu. Hata hivyo, masuala yanayoweza kuitwa sera ya uandishi na uchapishaji wa vitabu yanaweza kupatikana katika Tume za Elimu kadhaa zilizoundwa zinazoathiri uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada hasa katika mfumo wa elimu. Sehemu ifuatayo itaangazia historia ya uandishi na uchapishaji kwa kurejelea sera za elimu mbalimbali.

**Historia ya Uandishi na Uchapishaji Nchini Kenya**

Mnamo 1964 Serikali iliteua Tume ya Elimu ya Kenya iliyoongozwa na Profesa Ominde. Tume hiyo ilipendekeza mfumo wa elimu wa 7-4-2-3. Pia ikapendekeza Kiingereza katika kufundishia kuanzia shule za msingi. Aidha, ilipendekeza kukoma kwa ubaguzi shuleni na matumizi ya mtaala mmoja katika shule zote. Hata hivyo tume hii haikutoa mapendekezo yoyote kuhusu uchapishaji na upatikanaji wa nyenzo za ufundishaji .

Isitoshe ripoti ya Bessey (Republic of Kenya, 1972) ilipendekeza kuwepo kwa vitabu vya kiada zaidi ya kimoja kwa kila somo hasa katika shule za msingi na za upili, sababu iliyotolewa ni kuwa kuwepo kwa vitabu vya waandishi tofauti kungeshughulikia mada zile zile lakini kwa mtazamo tofauti na hivyo kuboresha ujifunzaji. Vilevile ikapendekezwa kuwepo kwa halmashauri maalum ya kukagua machapisho na kuyaidhinishwa kwa matumizi ya ujifunzaji na ufundishaji.

Tume ya Gachathi ya 1976 ilitoa mapendekezo yaliyoweza kugusia kiwanda cha uchapishaji. Pia iliweza kufahamu na kutambua umuhimu wa vitabu vya kielimu na hatua katika uchapishaji wavyo. Hivyo basi, ilikuwa vyema kuwepo muda ili kukamilisha mchakato wote wa uchapishaji ingawa wachapishaji wengi walikuwa ni wa kigeni ambao hawangeweza kutosheleza mahitaji ya wakenya kwa kuchapisha vitabu vinavyokidhi utamaduni na mfumo wa elimu. Tume ilitoa maoni juu ya hali hiyo iliyohitaji marekebisho.

Waaidha, Tume ya Gachathi ilichangia vitabu vya shule kuchapishwa na shirika la Jomo Kenyatta Foundation (iliyoundwa mnamo 1965). Shirika hili liliundwa hiki kiliundwa kwa madhumuni ya kupata faida zitakazotumiwa kuwapa elimu wanafunzi wanaotoka katika jamii za wasiojiweza.

Pia, Taasisi ya Elimu ya Kenya iliweza kuidhinisha matumizi ya vitabu vya Jomo Kenyatta Foundation (JKF). Hii ilikuwa mwanzo wa ukiritimba katika uchapishaji wa miswada ya TEK na JKF mnamo 1980, Kenya Literature Bureau iliundwa na kupewa mamlaka ya kupata miswada ya kielimu kutoka kwa TEK na kisha kuchapishwa.

Mnamo 1981 Tume ya Mackay iliundwa, Tume hii haikutaja jambo lolote kuhusiana na upataji wa vitabu bali ilipendekeza mtaala ambao unabobea mwelekeo wa kiufundi badala ya ule wa awali uliokuwa wa kinadharia. Mfumo wa awali ulimtayarisha mwanafunzi kuishinda mitihani tu na kutafuta kazi za utepemweupe. Ikapendekezwa kuwa mfumo wa elimu ubadilishwe kutoka 7-

4-2-3 hadi 8-4-4. Isitoshe, ili kuhakikisha kuwa ufundi umeifikia umma, ikatakiwa lugha ya Kiswahili isisitizwe. Hii ilitokana na ugunduzi kuwa wengi wa wanafunzi waliofuzu kutoka vyuo vikuu hawangeweza kujieleza kwa Kiswahili. Basi ikawa Kiswahili ni somo la lazima la kufundishwa na kutahiniwa katika mitihani ya shule za msingi na sekondari. Hata hivyo, mageuzi haya ya mfumo wa elimu yalipelekea uandishi na uchapishaji wa vitabu vipya, hivyo basi kupanua uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada ili kukidhi mahitaji ya shule zote nchini.

Uchapishaji wa vitabu vya kiada vya Kiswahili ulipata msukumo mkubwa mwaka wa 1985 Kiswahili kilipofanywa somo la lazima katika mfumo wa elimu. Vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, marejeleo, kamusi na vya fasihi vilichapishwa kwa wingi ili kukidhi soko la wasomaji shuleni Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (Kenya Institute of Curriculum Development) ilipewa jukumu la kukadiria ubora wa viwango vya miswada ya vitabu vya kiada kabla ya kuvichapisha ili vitumike shuleni kutokana na umuhimu wa vitabu hivyo kwa utekelezaji wa mtaala wa elimu.

Kabla ya mwaka wa 1991 jukumu la kuandika vitabu lilikuwa la serikali kupitia TEK. Awali kitabu kimoja cha kiada kilitumika kwa kila somo kwa shule zote nchini Kenya. Mnamo 1999, Tume ya Koech ilitoa mapendekezo yaliyosisitiza Kiswahili kufundishwa na kutahiniwa, haikugusia uchapishaji wa vitabu. Hata hivyo, mwaka huo huo Wizara ya Elimu ilipitisha sera mpya ya uchapishaji na uteuzi wa vitabu ambayo ilifanywa kuwa huria na jukumu la uchapishaji liliwachiwa wachapishaji binafsi. Aidha, sera mpya ilielekeza matumizi ya kitabu cha kiada zaidi ya kimoja.

Mnamo mwaka wa 2002, sera inayoelekeza utekelezwaji wa mtaala uliofanyiwa marekebisho ilitolewa, na ilihitaji TEK kiidhinishe vitabu sita vya kiada kwa kila somo katika kila darasa. Kutekelezwa kwa sera hii kulikusudiwa kuwapa wanafunzi na walimu mitazamo mbalimbali ya waandishi tofauti kuhusu dhana mbalimbali katika masomo. Mwalimu alitakiwa kuteua kitabu kimoja kutoka kwenye orodha rasmi ya TEK katika kijitabu kiitwacho *Orange Book* ili kitumike katika ufundishaji wa Kiswahili shuleni. Tume hizi zote zilitoa mapendekezo ambayo yalikuwa na athari kwa uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Kenya ambayo yatajadiliwa katika sura hii.

**Vitabu vya Kiada**
Mbunda (1983) anafafanua vitabu vya kiada kuwa ni vile ambavyo ndani mwake kuna maarifa na stadi kufuatana na malengo ya elimu katika Kiswahili. Stadi zenyewe ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Stadi hizi hufungamana na maarifa yanayohusu sarufi na msamiati. Stadi na maarifa haya hupangwa kwa utaratibu maalum kutoka kiwango cha chini hadi cha juu, kufuatana na mtalaa. Vitabu vya kiada hutimiza malengo ya mtalaa kwa kiwango fulani katika somo husika.

Vitabu hivi ndivyo uti wa mgongo katika uandishi na uchapishaji (Chakava, 1996; Makotsi na Nyariki 1997, Mulokozi, 1999). Vitabu vingi vya kiada nchini Kenya huteuliwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya. Vitabu hivi vilivyoteuliwa na kuidhinishwa vimewekwa kwenye kijitabu kinachoandaliwa na K I.C.D kiitwacho *Orange Book*; kulingana na Approved List of Primary and Secondary Schools Text-books and other Instructional materials, Revised 16th Edition (January, 2016). Kuna vitabu vya kiada vya kufundishia lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na katika shule za upili. Idadi hii inajumlisha vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu jinsi itakavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Makampuni ya Uchapishaji, Anwani za Vitabu na Idadi ya Vitabu vya Shule Vilivyoidhinishwa**

| Kampuni ya uchapishaji | Anwani ya kitabu | Shule za msingi | Shule ya upili |
|---|---|---|---|
| Longhorn Kenya | Msingi wa Kiswahili | 16 | -- |
| | Chemichemi za kiswahili | -- | 8 |
| Oxford University Press | Kiswahili Sarufi | 14 | -- |
| | Kiswahili Fasaha | -- | 8 |
| East African Educational Publishers | Masomo ya Msingi | 12 | -- |
| | Johari ya Kiswahili | -- | 4 |
| Macmillan Publishers(MK) | Nguzo za Kiswahili | 2 | -- |
| | -- | -- | -- |
| Evans Brothers (K) Ltd | Kina cha Kiswahili | 12 | -- |
| | -- | -- | -- |
| Kenya Literature Bureau | Kiswahili kwa Darasa | 8 | -- |
| | Kiswahili kwa Kidato | -- | 4 |
| Longman Kenya | Hazina ya Kiswahili | 2 | -- |
| | Longman Hazi ya Kiswahili | -- | 8 |
| Jomo Kenyatta Foundation | Tujivunie Kiswahili | 8 | -- |
| | -- | -- | -- |
| Moran Publishers | Moran Kiswahili Teule | 8 | -- |
| | Uhondo wa Kiswahili | -- | 6 |
| Longhorn (K) Ltd | Kiswahili Mufti | 14 | -- |
| | -- | -- | -- |
| Phoenix Publishers | -- | -- | -- |
| | Darubini ya Kiswahili | -- | 4 |
| Jumla | | 96 | 42 |

Kwa rejelea jedwali hili, vitabu hivi ndivyo vinavyoteuliwa na kutumiwa katika shule za msingi na upili nchini Kenya. Sehemu ifuatayo itashughulikia athari za uandishi na uchapishaji wa vitabu hivi tofauti tofauti katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Athari za Uandishi na Uchapishaji wa Vitabu vya Kiada aina aina vya Kiswahili**

Uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada tofauti tofauti vya Kiswahili una athari chanya na hasi kwa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili darasani. Kitabu cha kiada ni kitabu kinachotumiwa na mwalimu na mwanafunzi ambacho huwa na mpangilio maalum wa vipengele unao stahili kufuatwa.Aidha, kitabu cha kiada hupatikana kwa urahisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Pia hutumiwa kufanikisha malengo mahususi ya silabasi na malengo ya mtaala. Vitabu vya kiada tofauti tofauti humfanya mwalimu kuwa na upeo mpana kwa sababu anaweza kulinganisha na kulinganua matini yanayopatikana katika vitabu mbalimbali. Hivyo basi, kuibuka na kazi iliyo na mpangilio mwafaka ambao utawafanya wanafunzi kumwamini mwalimu anapowasilisha kazi yake darasani.

Aidha, vitabu vya kiada hushughulikia mahitaji ya mwanafunzi. Matumizi ya vitabu vya kiada tofauti tofauti husababisha mwalimu kufanya maandalizi ya somo mapema, ataweza kuandaa maazimio akiwa na umakinifu wa kuchagua mbinu faafu atakayotumia katika ufundishaji wake. Halliwel (2006) anasema kwamba vitabu vya kiada humsaidia mwalimu kutoa ratiba ambayo ina muundo na mtitiriko mwafaka unaojumuisha mwendelezo wa mazoezi. Aidha vitabu hivyo husaidia kutimiza au kuafikia mahitaji ya mwanafunzi na humwezesha mwalimu kugawanya kazi yake ili aweze kuwa na mpangilio mwafaka kwa mwaka mzima.

Athari nyingine ya uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada tofauti tofauti ni kuwa wanafunzi wanaweza kufanya mazoezi na tamrini za kutosha kutokana na vitabu vya kiada vingi. Hivyo basi mwalimu ataweza kukadiria utekelezwaji wa madhumuni ya somo (Litz, 2000). Kuwemo kwa mazoezi toshelevu kitabuni humsaidia mwanafunzi kupima weledi wa dhana alizofunzwa na huchangia katika kumuandaa kwa mitihani ya kitaifa. Kwa mujibu wa Crisp, Anderson, Orme na Lister (2005), vitabu vya kiada humwezesha mwanafunzi kujifahamisha kuhusu mada, dhana, mitazamo, stadi na maadili yanoyompasa kujifunza katika mtaala wa somo.

Pia, vitabu vya kiada vimeathiri mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kutokana na hali kuwa, kuwepo kwa vitabu tofauti tofauti kumemfanya mwalimu kuwa mtafiti na mweledi wa dhana mbalimbali zilizotumika, hivi kwamba mwalimu hufanya utafiti wake mapema ili kutambua ufafanuzi na maelezo yaliyopewa katika vitabu hivi tofauti tofauti. Mwalimu na mwanafunzi wanaposoma vitabu tofauti kuhusu mada ile moja, wanapata mitazamo tofauti kuhusu mada ile moja, kutokana na waandishi tofauti (Kochhari, 1991), Mwalimu wa somo la Kiswahili ana uhuru wa kupanga na kupangua mada kitabuni wakati anapofunza ili somo lake liwe na mtiririko mzuri.

Aidha, uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada aina aina umechangia kuibuka kwa waandishi chipikuzi pamoja na makampuni ya uchapishaji kinyume na hapo awali wakati jukumu lote la uchapishaji lilikuwa limeachiwa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya. Kuna baadhi ya wadau walio na dhana kuwa vitabu vilivyochapishwa na makampuni ya awali kama vile JKF na Kenya Literature Bureau (KLB) ndivyo vitabu vinavyofaa katika ufundishaji. Hivyo basi, vitabu vya makampuni haya huteuliwa na kununuliwa katika shule mbalimbali ilhali vitabu vya makampuni mengine vikikosa soko.

Ijapokuwa vitabu vya kiada vina athari chanya katika ufundishaji wa Kiswahili, hata hivyo vina athari hasi pia kwa sababu zifuatazo: Matumizi ya vitabu vya kiada tofauti tofauti vimewafanywa walimu wategemezi na kukosa ubunifu kwa sababu wana wajibu wa kufuata mpangilio uliyomo katika kitabu kwa mujibu wa mtaala (Ur, 1991). Aidha, kuna ubanifu katika upanuzi wa mawazo kwa sababu vitabu hivi aina aina humpa mwanafunzi mazoezi, ufafanuzi na mifano ya kutosha. Hivyo basi mwalimu haoni haja ya kutunga na kuandaa mazoezi zaidi yake binafsi.

Pia, matumizi ya vitabu vya kiada tofauti tofauti hutatiza weledi wa dhana (Muhammed na Kumari, 2007). Baadhi ya vitabu vya kiada huwakanganywa wanafunzi kutokana na ufafanuzi wa dhana unaotofautiana wa waandishi mbalimbali. Mwalimu anakuwa na wakati mgumu kuwapa maelezo faafu kuhusiana na utofauti huo.

Isitoshe, sera ya kuidhinishwa kwa vitabu sita vya somo la Kiswahili kwa kila darasa imezua athari chanya na hasi. Athari hasi ni kuwa wakati wa uteuzi wa kitabu cha kiada kuna kamati inayoshughulikia jambo hilo na katika shule ambako mwalimu anayesimamia Idara ya Lugha hakuwa mwalimu wa Kiswahili, kuna uwezekano wa kuteua kitabu cha kiada kisicho mwafiki

mtumiaji. Hivyo basi, mwalimu wa Kiswahili anatakiwa kuhusishwa katika uteuzi wa kitabu cha kiada moja kwa moja ili apate ufahamu wa kina kuhusu kitabu husika kabla ya kukiteua.

Chambers (1997) anadokeza kuwa hakuna njia ya moja kwa moja ya kuchagua au kuteua kitabu cha kiada faafu cha ufundishaji, ni kazi ngumu hivi kwamba katika kutathmini vifaa vya ufundishaji kuna sababu za kurejelewa kama vile umri wa mwanafunzi, utamaduni ufaao, mbinu za ufundishaji, kiwango na thamani yake, idadi na aina ya mazoezi, ujuzi, mwongozo wa mwalimu, mwendo, aina, ujumuishaji wa anayefundisha na utatuzi wa masuala. Illes (2009) anasema kuwa soko la vitabu vya kiada limefurika, hiyo basi ni vigumu kwa mwalimu kuchagua kitabu faafu kinachokidhi mahitaji ya mwanafunzi kwa mujibu wa silabasi. Ni wazi kuwa ukosefu wa uhamasishaji wa walimu kuhusu kutathmini vitabu vya kiada kumefanya walimu kuchagua vitabu tu bila kuvichunguza. Ni vyema semina au warsha ziwepo pamoja na waandishi na wachapishaji mbalimbali ili walimu waweze kuuliza maswali. Katika utafiti wetu tuliofanya tulibaini kuwa kati ya shule 28 ni shule mbili tu ndizo zilitumia nakala tofauti ya kitabu cha kiada. Shule nyingi hutumia kitabu cha kiada aina moja tu.

Vilevile, athari nyingine hasi inayojitokeza katika uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada tofauti tofauti ni kuwa kila kitabu kimeainisha mbinu tofauti tofauti ya ufundishaji. Hivyo basi, inakuwa vigumu kwa mwalimu kuchagua kitabu cha kiada atakachotumia. Katika muktadha wa kitabu cha kiada aina fulani kutumika katika shule husika itamlazimu mwalimu huyo kutumia mbinu iliyomo katika kitabu teule. Hali hii hubana mwalimu katika ufundishaji wake.

Katika matumizi ya vitabu vya kiada tuligundua kuwa dhana kuwa makampuni ya awali kama vile JKF na KLB ndiyo bora katika uchapishaji wa vitabu, imewafanya walimu kuchagua na kupendelea, kununua na kutumia vitabu vya kiada tu vilivyoandikwa na kuchapishwa na makampuni hayo. Hivyo basi, vitabu vya makampuni mengine hukosa soko la vitabu vyao. Aidha, baadhi ya walimu hutegemea sana kitabu cha kiada kimoja bila kurejelea vitabu vingine kutokana na matini yanayopatikana katika kitabu husika.

**Hitimisho**

Azma ya sura hii ilikuwa ni kuchunguza namna uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada tofauti tofauti umeathiri ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi na za upili. Kutokana na mjadala ni kweli kuwa vitabu vya kiada ni uti wa mgongo katika kuinua kiwango cha elimu. Aidha, matumizi ya vitabu vya kiada tofauti tofauti ya athari kubwa kichanya au kihasi katika ufundishaji wa Kiswahili. Inadhihirika kuwa uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada tofauti tofauti imemfanya mwanafunzi na mwalimu kupata mitazamo ya waandishi tofauti kuhusu dhana moja. Mwalimu anastahili kutumia vitabu vyote vya kiada katika maandalizi ya somo analolifunza, jambo ambalo litawafanya wanafunzi kujenga imani kwa mwalimu wao.

## Marejeleo

Altbach, G. P. (1999). The Dilemmas of Publishing in African Languages: A Comparative Perspective. In P. G. Altbach and D. Teferra (eds.), *Publishing in African Languages: Challenges and Prospects.* Chestnut Hill: Bellagic Publishing Network. Pg. 1-10 .

Chambers, F. (1997) Seeking Consensus in Coursebook Evaluation. *ELT Journal*, 51, 29-35.

Chakava, H. (1996). *Publishing in Africa :One Man's Perspective.* Nairobi: EAEP.

Crisp, B. R., Anderson, M. R., Orme, J. & Lister, P. G. (2005). *Learning and Teaching in Social Work Education: Textbooks and Frameworks on Assessment.* University of Glasgow

Halliwel, S. (2006). *Teaching English in a Primary Classroom.* Harlow: Pearson Education Ltd.

Illes, E. (2009). What makes a coursebook Series stand the test of time? *ELT Journal*, 63(2) 145-153.

Ipara, I. O. (2007). *Oral Questioning in the Pedagogy of Kiswahili Grammar: A Study of Teachers Practices in Selected Secondary Schools of Bungoma District, Kenya* Unpublished Phd.Thesis, Moi University. Eldoret

Kochhari, K. S. (1991). *The Teaching of Social Studies* New Delhi: Sterling Publishers Limited.

Litz, D. R. (2000). Textbook Evaluation and ELT management :A South Korean Case study. *The Asian EFL Journal.* Retrieved from: | http://www.melta.org

Makotsi, R., & Nyariki, L. (1997). *Publishing and Booktrade in Kenya.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbunda, F. (1983). Misingi ya Uandishi wa Vitabu vya Kiada katika *Makala za Semina ya Kimatafa ya Waandishi wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Ministry of Education. (2016). *Approved List of Primary School Textbooks and other Instructional Materials.* Nairobi: MOEST.

Ministry of Education (2016). *Approved list of Secondary School Textbooks and other Instructional_Materials.* Nairobi: MOEST.

Muhammad, R. F., & Kumari, R. (2007). Effective Use of Textbooks: A Negelected Aspect of Education in Pakistan. *Journal of Education for International Development*, 3:1.Retrieved from: http://www.equip123.net

Mulokozi, M. M. (1999). Publishing in Kiswahili: A Writers' Perspective. In P. G. Altbatch & D. Teferra (Eds.), *Publishing in African Languages: Challenges and Prospects.* Chestnut Hill: Bellagio Publishing Network. PP. 11-4 2

Ogechi, N. O. (2004). Athari za Mabadiliko ya Mtaala ya Kiswahili katika Uandishi na Uchapishaji, katika *Swahili Forum 11.* Web publication at www.ufeas.uni – mainz.de/swafo/sf//

Republic of Kenya. (1972). *A Study of Curriculum Development in Kenya* (Bessey Reports). Nairobi: English Press.

Rotich, D. C. (2006). *Publishing and Distribution of Educational Books in Kenya: A Study of Market Liberalisation and Book Consumption.* (Unpublished PhD Thesis, Thames Valley University, London).

Ur, P. (1991). *A Course in Language Teaching: Practice and Theory.* Cambridge: Cambridge University Press.

# SURA YA ISHIRINI NA TISA

## Maandalizi ya Walimu wa Kiswahili Nchini Uganda

Anne Nabutola Wanjala[1], Misiko Wasike[1], Isaac Odeo Ipara[1] na Carren Nyandiba[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Kibabii*
[2]*Chuo Kikuu cha Rongo*

**Utangulizi**

Ufundishaji wa somo la lugha ya Kiswahili unahitaji walimu waliohitimu katika mbinu mwafaka za ufundishaji. Maandalizi hayo ni muhimu zaidi hususan katika nchi ambapo Kiswahili, kwa muda mrefu, hakikupewa hadhi kinachostahili kama Uganda. Ni kutokana na umuhimu huo ambapo sura hii ianaangazia umuhimu wa maandalizi ya walimu wa somo la Kiswahili nchini Uganda na nafasi yake katika kujenga sifa za mwalimu bora. Suala la uwajibikaji wa walimu katika ufundishaji limetiliwa mkazo na washika dau. Ufaafu wa walimu kwa kiasi kikubwa unapimwa kupitia kwa matokeo ya mitihani ya wanafunzi. Wasimamizi wa shule wana changamoto ya kuhakikisha kuwa walimu waliohitimu ndio watakaosimamia kila darasa. Kwa mwelekeo huo basi, wasimamizi hao wanapaswa kutambua sifa za mwalimu bora. Kwa mujibu wa Barnes na Aguarrebere (2006), tathmini ya ubora wa walimu inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: undani wa uelewa wao wa mada; ubora wa kubadilisha uelewa huo kwa kuwaelekeza wanafunzi wa umri tofauti tofauti, na wenye uwezo unaotofautiana; na uwezo wao wa kuoanisha michakato yote ya darasa.

Mukama (1989) anasema kuwa Kiswahili kinachangia sana kwa kuwaunganisha wananchi katika ukanda wa Afrika Mashariki na hivyo kuimarisha ushirikiano wa Afrika Mashariki. Naye Muthwii (2002) anatetea nafasi ya Kiswahili katika ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kusema kuwa Kiswahili kina nafasi ya kipekee katika mazingira ya biashara, dini, vyombo vya habari, utawala na ajira. Anaendelea kusema kuwa, Kiswahili hutumiwa kama *Lingua Franka* na kama chombo cha kuwaunganisha pamoja na kuwatambulisha Waafrika. Hivyo basi ili kuimarisha na kudumisha juhudi zinazotekelezwa na mataifa mbalimbali katika ushirikiano wa Afrika Mashariki, katika harakati za kukuza na kueneza Kiswahili, serikali ya Uganda haina budi kuhakikisha kwamba kuna sera maalumu inayodhibiti matumizi ya Kiswahili. Mikakati imewekwa ili kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kwa mujibu wa mkaguzi wa elimu katika Kaunti ya Bugiri, serikali imeteua shule tatu ambazo kwazo inafanya majaribio ya ufundishaji wa Kiswahili ili ipate kuanzisha masomo rasmi ya Kiswahili katika nchi ya Uganda.

Sura hii ni matokeo ya utafiti mdogo uliofanywa kuhusu mitazamo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Aidha, uchunguzi huo ulitathmini haiba ya walimu na vitabu vinavyotumika katika kufunza Kiswahili nchini humo. Maendeleo ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda yamekuwa na changamoto sana ikilinganishwa na nchi za Tanzania na Kenya. Sura hii ianatangulizwa kwa uhakiki wa sera ya lugha nchini Uganda na kisha kujadili maandalizi ya walimu, mitazamo ya walimu kuhusu ufundishaji, haiba ya mwalimu katika ujifunzaji na vifaa na mbinu za kufundishia.

**Sera ya Lugha Nchini Uganda**

Katika nchi ya Uganda kama ilivyo katika nchi nyingi za Kiafrika, Kingereza ambayo ni lugha ya utawala wa kikoloni ilipewa kipaumbele katika serikali na umma kupitia uinjilisti, na elimu. Katika miongo ya kwanza ya karne ya ishirini, Kiswahili kilipata umaarufu kwa kuwa, kando na kutumiwa na jeshi na polisi, pia kilifundishwa shuleni. Nchi ya Uganda ilipopata uhuru mwaka wa 1962, Kingereza kilibaki kuwa lugha rasmi. Waganda waliona kuja kwa Kiswahili kama tishio kwa nguvu zao za kisiasa kwa kiasi kikubwa. Kingereza basi kilibaki kuwa lugha rasmi ya pekee. Hali ya wingi lugha ya Uganda ilifanya ikawa vigumu kuchagua lugha nyingine kama lugha rasmi ya Uganda.

Baada ya uhuru, kulikuwa na juhudi za kuteua lugha asilia kuwa rasmi. Luganda na Kiswahili ndizo lugha zilizoangaziwa sana. Ingawa Luganda ilikuwa imeenea sana kijiografia, wenyeji wasio Waganda, waliipinga kuwa lugha ya taifa. Vilevile wale wa ufalme wa Buganda nao pia walipinga pendekezo hili kwa sababu walihisi kuwa makosa ya kimatamshi na sarufi kutoka kwa watu wa makabila mengine yangeharibu lugha yao ya 'kifalme'. Basi Kiingereza kikabakia kuwa lugha ya taifa. Wakati wa utawala wa rais Idd Amin, Kiswahili ambacho kilikuwa *Lingua Franka* ya Afrika Mashariki kilifanywa kuwa lugha ya pili ya kitaifa, ingawa baadaye hadhi yake ya utaifa ilipotea kwa mujibu wa katiba ya 1995. Baadaye tena, mnamo Septemba 2005, bunge la Uganda lilipigia kura Kiswahili kuwa lugha ya pili rasmi. Ukweli ni kwamba urasmi huu wa Kiswahili unatiliwa shaka na wataalamu wengi wa Kiswahili kwa kuwa tokeo hili halijatiwa rasmi katika katiba ya nchi ya Uganda. Kwa mujibu wa Mukuthuria (2006), ili kuimarisha na kudumisha juhudi zinazotekelezwa na mataifa mbalimbali katika ushirikiano wa Afrika Mashariki, katika harakati za kukuza na kueneza Kiswahili, serikali za Afrika Mashariki zikiwemo Uganda zina wajibu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba kuna sera maalumu inayodhibiti matumizi ya Kiswahili.

**Maandalizi ya Walimu**

Maandalizi ya walimu yanarejelea mafunzo wanayopewa wakiwa vyuoni ili kuwatayarisha kwa ajili ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili. Kwa mujibu wa Mpunga (2003) uwezo wa mwalimu hubainisha kiwango cha elimu na ujifunzaji. Laczko-Kerr na Berliner (2003) katika utafiti waliofanya kuhusu ufundishaji waligundua kuwa walimu walijifunza vyema zaidi kama mfumo wao wa maandalizi ulijikita kwa mada katika somo, sayansi na sanaa ya ufundishaji ikihusisha nadharia za ujifunzaji, nadharia za ukuaji, nadharia za umotishaji na habari za utahini wa wanafunzi pamoja na ukurufunzi wa ufundishaji. Uamuzi kutokana na utafiti wa wataalamu hawa ulionyesha kuwa kuajiri mwalimu aliyehitimu kulitoshana na kukamilisha asilimia kumi ya mwaka wa masomo. Hivyo wanafunzi walipoteza asilimia 20 ya makuzi ya kielimu kila mwaka kwa kuwa na mwalimu ambaye hakuhitimu. Kwa kuzingatia mawazo ya wataalamu hao, basi kuna changamoto kwa baadhi ya walimu wa Kiswahili nchini Uganda ambao hawakusomea ualimu, wala ufundishaji wa somo la Kiswahili.

Darling-Hammond na Berry (2006) wanasema kuwa, cheti cha walimu cha kuhitimu kimsingi kinamaanisha kuwa mwalimu ameandaliwa katika programu za kielimu zilizoidhinishwa na taifa kwa kiwango cha stashahada au shahada na amekamilisha kiwango cha alama 18-40, na majuma 8-18 ya mazoezi ya kuwafunza wanafunzi. Baadhi ya walimu nchini Uganda hawajapata shahada wala stashahada katika ualimu, mbali na kuhitimu katika lugha ya Kiswahili. Inapendekezwa kuwa serikali itambue kwamba changamoto yake kuu ni kuandaa walimu wanaoweza kuvumbua, kuwaza na kutathmini mbinu za ujifunzaji, na wale wanaoweza kukabiliana na hali yoyote ngeni pindi itokeapo. Haya yatatekelezwa iwapo mwalimu atapata maandalizi chuoni na nyanjani. Akiongezea umuhimu wa mwalimu kuandaliwa awali, Porter-Magee (2004), anadai kwamba

utafiti umeendelea kuonyesha kuwa walimu wenye msingi imara kimasomo, wana athari zaidi kwa yale wanafunzi wao wanajifunza. Burudi (2009) akishadididia umuhimu wa maandalizi ya walimu anakubaliana kuwa walimu walioingilia taaluma zao bila kuandaliwa kisayansi na katika sanaa ya ufunzaji walikuwa na ugumu wa kupata mbinu na vifaa ainati walizokuwa nazo walimu bora. Kwa kuzingatia maoni ya wasomi hawa, tunahoji kuwa maandalizi wanayopewa walimu wanaofunza Kiswahili katika nchi ya Uganda yanapaswa kuimarishwa zaidi. Ujifunzaji wa kweli hutokea vigezo maalum vikitekelezwa. Vigezo ni seti tofautitofauti za hali zinazojitokeza ambazo zinastahili kutimizwa ili ujifunzaji utokee. Mwalimu ni kigezo maalum kimoja. Basi inafaa walimu wanaofunza Kiswahili katika shule za Uganda waandaliwe vilivyo. Ufundishaji unamaanisha kutayarisha mazingira ya ufunzaji na ujifunzaji ambayo yataathiri anayejifunza. Mwanafunzi anastahili mafunzo faafu katika mada husika. Hivyo basi maandalizi ya walimu ni muhimu wanapokuwa vyuoni au nyanjani ili yawasaidie kuhakikisha kuwa mwanafunzi ana umilisi wa kiwango cha chini kabla ya kupata ujuzi wa viwango vya juu.

**Mitazamo ya walimu katika ufundishaji**

Mtazamo ni hisia za kupenda au kutopenda kitu, hapa tukirejelea somo la Kiswahili nchini Uganda. Katika sura hii tunahoji kuwa walimu ambao wameandaliwa barabara wanapaswa kuwa na mtazamo wa kupenda kutumia na kufundisha somo la Kiswahili. Ndoleriire, (1996) akichangia umuhimu wa maandalizi mema anasema kuwa maandalizi ya walimu hutambuliwa kama mbinu ya kukuza mitazamo chanya kuhusu masomo yanayofunzwa shuleni. Maandalizi huleta ujuzi, maarifa na mitazamo inayohitajika kwa kazi na majukumu. Nchi ya Uganda inaazimia kuanzisha masomo rasmi ya Kiswahili ambayo ni mabadiliko muhimu katika mtalaa ambapo kwa sasa Kiswahili si somo la lazima. Kwa mujibu wa Anderson (2004), utekelezaji wa mpango mpya wa elimu hufaulu iwapo mitazamo ya walimu na wanafunzi imeshughulikiwa kupitia kwa maandalizi ambayo yatawasaidia katika uteuzi wa nyenzo faafu za kufundishia, kuiga mielekeo chanya katika ufundishaji na kutumia utendaji katika mafunzo ili kupatia somo uhai. Vivyo hivyo, mwalimu ambaye hajaandaliwa vilivyo atakuwa na mtazamo hasi ambao utatinga ufundishaji.

Mitazamo ya walimu wa wilaya ya Bugiri inapaswa kushughulikiwa ipasavyo ili kukidhi mahitaji ya kufundisha Kiswahili ambalo ni somo jipya kwa kiasi kikubwa nchini Uganda. Ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda unakabiliwa na matatizo kwa sababu walimu wengi hawana ufahamu mzuri wa mada za somo la Kiswahili, na pia hawakuandaliwa ipasavyo nyanjani ili wajifahamishe na mambo mapya kuhusu somo hilo. Hali hii huwafanya wakate tamaa, na hatimaye huathiri utekelezaji wa silabasi ya somo la Kiswahili. Ufundishaji wa Kiswahili huhitaji wataalam wa hali ya juu na wenye kujitolea ili wawavumilie wanafunzi wanaochukua muda mrefu kupata mielekeo faafu katika somo hili. Walimu wanaofunza Kiswahili Uganda wanapaswa kuandaliwa kwa njia ambayo inawawezesha kukuza mtazamo wa kuwavumilia wanafunzi. Walimu wengi wa wilaya ya Bugiri nchini Uganda hawaandaliwi kupitia kwa kozi za kujipiga msasa pamoja na warsha na makongamano. Mara nyingi hawapati habari kuhusu warsha ama hupata habari wakiwa wamechelewa. Ni kweli kuwa viwango vya kuhitimu na tajriba ya walimu vinatakikana kuwa na ufungamano na utekelezaji wa ufundishaji wa somo la Kiswahili nchini Uganda. Nia mbovu ni kikwazo mojawapo cha ujifundishaji mwafaka wa lugha. Walimu wanapaswa kujenga nia nzuri ya kukipenda Kiswahili na kukikuza vilevile. Hili watalijenga kupitia maandalizi mema katika ujifunzaji wao wa ualimu na hususan ualimu wa Kiswahili.

**Haiba ya Mwalimu katika Ufundishaji**

Sura hii inahoji kuwa mwalimu ambaye ameandaliwa vyema anapaswa kuwa na haiba inayojenga ufundishaji wa Kiswahili. Haiba ya mwalimu ni kigezo muhimu na cha kati katika hulka ya mwalimu. Haiba hufasiriwa kama sifa spesheli na maalum za kibinafsi za mwalimu. Ukati wa mwalimu katika ufunzaji na ujifundishaji ni kama daraja kati ya ufanisi wa mwanafunzi na ufaafu wa mwalimu, na hutambulika kwa mapana. Kutokana na ratiba au mfumo ulioundwa na, Garret (2009), Walker (2008), kuna sifa muhimu ambazo zinahusiana na haiba ya mwalimu. Sifa hizi zimeelezewa ifuatavyo: Kwanza, mwalimu bora anapaswa kujiamini. Bandura (1977), anafasili kujiamini kama uwezo wa kiakili unaomwezesha mtu kujenga imani yake kuhusu uwezo wake wa kufikia kiwango fulani cha utimilifu au ufanisi. Hii ni nia ya kujua anaweza. Mwalimu kama huyo huwa amejipiga msasa na anaweza kujieleza vyema. Kuongezea hayo, mwalimu mzuri ni mwenye huruma, hutambua changamoto za kibinafsi za wanafunzi na hivyo hawaaibishi kwa kukosoa upungufu wao hadharani darasani. Isitoshe, mwalimu mzuri ni mcheshi, hucheka kwa urahisi, huchekesha, huleta wepesi, na hufanya utani darasani. Ni mwenye kujali wanafunzi na anayeitikia na kuelewa hali iliyopo. Anajihusisha kibinafsi na wanafunzi. Ana nia chanya na mwelekeo unaoamini kuwa anayodhamiria yanawezekana.

Pili, ni kuwa mwalimu mzuri sharti awe na ari na mwao wa kufunza. Awe anafurahia kufunza na ana msukumo wa mvuto kwa mada. Adhibiti vilivyo kazi na ulingo wake. Mwalimu huyo aonyeshe utendaji wa kifasaha wa hali ya juu katika maongezi na maandishi yake. Mwalimu bora ni nguzo kwa wanafunzi. Anaonyesha upendo na ana mikakati ya kuwasaidia wanafunzi kupenda kutenda kwa kuwasifu na kuonyesha kuwa anatambua juhudi zao. Mwalimu bora hutia nguvu kwa kazi na huwavutia wanafunzi kumfuata. Huwa na ujasiri na ni mtulivu hivyo hufanya wanafunzi kutulia. Mwalimu bora hudhihirisha uongozi na huwatia motisha wanafunzi. Yeye hukiri anapokosa na kuonyesha hisia za kibinafsi zinazogusa wanafunzi.Vile vile ni nadhifu katika mpangilio wa kazi. Haiba ya mwalimu wa Kiswahili nchini Uganda ni muhimu katika ujifunzaji wa wanafunzi na huchangia ufanisi wao. Ufanisi wa wanafunzi hapa unafasiriwa kama kupata alama za juu kwa mitihani, makuzi ya kimasomo na kunawiri, ukomavu kwa mahusiano ya kijamii na pia uwezo wa kukabiliana na hali tata. Anderson (2004), anashikilia kwamba walimu bora ni wale ambao wanafuatilia na kukamilisha mahitaji na malengo ya kisilibasi ili kuwawezesha wanafunzi kutimiza malengo yaliyowekwa.Walimu hawa huweza kujieleza waziwazi. Sifa ya kuwezesha mtagusano ni muhimu kwa mwalimu. Aidha, mafunzo nyanjani yanasaidia kumpa mwalimu tajiriba na kumfahamisha mambo mapya ya hivi karibuni katika somo lake. Hali hii huwa na athari chanya miongoni mwa walimu. Walimu wa Uganda wanafaa kuandaa warsha za kujadili maandalizi yao ili waelewe hali yao na pia kuweza kushughulikia maswala ibuka yanayodhihirika katika mazingira yao, kama vile haki za kijinsia na janga la ukimwi ambayo yanaweza kuathiri ufunzaji wao kwa namna moja au nyingine.

Odeo (2003) na Egessa (2007) wanaona kwamba kikwazo kimoja kwa ufundishaji na ujifunzaji bora ni sifa za kibinafsi za mwalimu. Hivyo basi, tunaposherehekea wasomi na ujuzi wa karne ya ishirini na moja katika uwezo, maarifa, maadili na uelewa, pia tunapaswa kuzingatia sifa za walimu wao. Wazo la kimsingi linalorejelewa katika sura hii ni kuwa sifa za kibinafsi huathiri na kuamua vipengele vyote vya mwalimu vikiwemo mbinu za ufundishaji, ujuzi wa kitaaluma, matendo na nia yake. Kwa kuzingatia mambo haya, inapendekezwa kuwa sifa za kibinafsi za walimu wa Kiswahili nchini Uganda zikuzwe kupitia kwa maandalizi vyuoni. Cha muhimu zaidi ni kwa walimu wanaofunza Kiswahili nchini Uganda kutambua umuhimu wa sifa zao za kibinafsi katika ufunzaji wao wa Kiswahili. Uelewa wa mwalimu wa Kiswahili wa lugha nenwa na andishi unapaswa kuwa usiotiliwa shaka. Haya yatawapa walimu ujasiri wa kuwawezesha kuwa kielelezo bora ipasavyo. Ni muhimu kwa walimu wa Kiswahili nchini Uganda kuboresha

haiba zao za kibinafsi ili kupata heshima ya wanafunzi wao. Mapendekezo haya yote yanalenga haiba inayojitokeza ya mwalimu kama vile kupaza sauti, ufahamu, mpangilio nadhifu, ari, ucheshi, mwitikio na mvuto.

Kwa vile hali ya Kiswahili nchini Uganda ni tata, uwepo wa mwalimu mwenye haiba faafu darasani ni muhimu. Kangahi (2016) anasema kuwa ufundishaji mzuri na matokeo yaliyoboreshwa hutokea ikiwa kuna uwiano kati ya njia ya ufundishaji na ujifunzaji. Anasema kuwa mbinu zisizofaa, na zile zisizotilia maanani uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi huleta matokeo duni. Hali hii inabainika nchini Uganda kwa sababu ya ukosefu wa uwaino huu. Awali, Burudi (2009) alidai kuwa walimu kwa nadra sana hutumia viziada lugha kama vile ishara za mikono wanapofunza Kiswahili kwa vile hawaelewi athari za ishara hizo kwa mazingira ya masomo. Tunahoji kuwa walimu wanaofunza Kiswahili nchini Uganda wakuze haiba itakayowaruhusu kutumia ishara mbalimbali inavyostahiki. Uchunguzi wa Koteng (2009) ulibainisha kuwa kulikuwa na uhusikaji mdogo wa wanafunzi darasani kwa sababu ya mtindo wa mawasiliano ya kumoja kutoka kwa mwalimu kuelekea kwa wanafunzi. Wanafunzi walikosa umotishaji ambao husababisha mwitikio kutoka kwao. Koteng basi anakubaliana na Odeo (2003), kwamba ingawa wanafunzi hushiriki sana kwa mawasiliano nje ya darasa, wao hunyamaza kimya wakati wa ufundishaji wa darasani kwa sababu ya kukosa motisha. Walimu nchini Uganda wanapaswa kuunda mazingira ya kusoma ambamo wanafunzi wanaweza kushiriki kikamilifu na kwa usawa.

Mafunzo ya ualimu husaidia kumtayarisha mwalimu kushiriki katika mfumo wa elimu ya nchi yake kikamilifu kwa kumpa umilisi wa kiakademia, stadi maalum na mwelekeo unaofaa. Elimu ya ualimu imepangwa kutayarisha mtu ambaye anaelewa ulimwengu unaomzunguka na anaweza kufikiri na kufanya kazi kimantiki. Ripoti hii inapendekeza kuwa walimu wanaohudumu wapewe mafunzo zaidi ili waweze kushirikisha teknolojia mpya katika ufundishaji wao. Kwa kuzingatia mawazo haya tunahoji iwapo vyuo vinavyowatayarisha walimu wa Kiswahili nchini Uganda vinawapa matayarisho yanayowafaa. Taaluma ya Kiswahili kama ilivyo ya masomo mengine inatarajiwa kuandaa na kufundisha kozi ambazo zinakubaliana na matarajio, pamoja na mabadiliko katika jamii huku ikizingatia mitaala ya asasi za mafunzo hasa shule. Matayarisho ya walimu wanaofunza Kiswahili nchini Uganda yanapaswa kuzingatia mabadiliko haya katika jamii.

**Vifaa na Mbinu za Kufundishia**

Walimu wa Kiswahili nchini Uganda ikiwa wameandaliwa ipasavyo wanapaswa kutumia mbinu mwafaka katika ufundishaji wao. Mkazo uwe kwa mbinu za mtagusano. Hivyo walimu watakuwa huru darasani na kukuza mazingira ya kirafiki ambayo yatafanya ujifunzaji kuwa wa kuvutia. Nchini Uganda, kama kwingineko, madarasa mara nyingi hayatoi mazingira ya kujifunzia yanayofaa kwa sababu ya mpangilio wake. Kwanza, vifaa vya kufundishia somo la Kiswahili ni vichache, na tena ni jukumu la mwalimu kuvitafuta mwenyewe. Tatizo lingine ni lile la wanafunzi kuketi wakitazama mbele, hali inayokwamiza mtagusano miongoni mwao. Ili kufanya somo la Kiswahili livutie wanafunzi nchini Uganda, hasa kwa kuwa ni somo geni, mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ili kulipa somo lake uhai; anastahili kutumia vifaa vya ufundishaji vya kuvutia; kubadili mandhari ya darasa na shughuli za darasani ili kufanya mazingira yavutie.Vilevile, mwalimu anahitajika kutumia teknolojia kama vile mtandao na vifaa tamba kama rununu ambavyo ni maarufu mno kwa wanafunzi. Nyenzo hizi zitaimarisha mtagusano wa mwalimu na wanafunzi.

Dornyei, (2009) anasema kwamba wakati mabadiliko yanapofasiriwa kwa njia isiyofaa, huwafanya walimu kutotilia maanani utaratibu uliowekwa na kwa hivyo mikakati na mbinu za ufundishaji zilizopendekezwa huenda zikapuuzwa. Ilivyobainika, walimu wengi wa Kiswahili wilayani Bugiri hawana silabasi ya somo hilo na zaidi hawahudhurii warsha zozote kuhusu mabadiliko ya kisilabasi kwa sababu hawapati mialiko kwa wakati unaofaa Koteng (2009) aligundua kuwa vyuo vikuu pia havina utaratibu sawia wa kutayarisha walimu, na basi kila mwalimu hufunza kulingana na jinsi alivyofunzwa chuoni kwa kutumia mtalaa wa chuo chake. Ukweli ni kwamba, walimu wengi wanaofunza Kiswahili katika kaunti ya Bugiri nchini Uganda wameandaliwa nchini Kenya, licha ya kwamba mtaala wa somo la Kiswahili nchini Uganda ni tofauti na ule wa Kenya, kwa sababu ambazo zinaeleweka. Kuna uwezekano wa mwalimu huyu aliyeandaliwa Kenya, kuwa mmilisi wa lugha lakini akakosa uwezo wa kuwasilisha elimu hiyo kwa mwanafunzi wa wilaya ya Bugiri kwa sababu ya ukosefu wa mbinu mwafaka za kutekeleza ujifunzaji wa Kiswahili katika mazingira ya Uganda. Pia, kwa sababu ya nafasi ya Kiswahili nchini Kenya, kiwango cha mafunzo yake ni cha juu kwa mwanafunzi wa Wilaya ya Bugiri nchini Uganda kwani mitaala ya Kiswahili ya nchi hizi mbili si sawa.

Kwa walimu ambao wameandaliwa nchini Uganda, wengi wao wametayarishwa kufunza masomo mengine lakini kwa kuwa wanakifahamu Kiswahili kidogo, na wanataka ajira, wao huishia kukifunza Kiswahili bila mafunzo maalum. Walimu hawa 'bandia' wa Kiswahili wanapaswa kusoma zaidi na pia kuhudhuria mafunzo mwafaka ili waweze kufunza Kiswahili ipasavyo. Sifuna (1989) anashikilia kuwa, mwitikio maalum hutolewa na mwanafunzi kwa kichocheo kama picha, michoro, au kichwa cha mada kitabuni. Mwitikio huo utatokea tu ikiwa wanafunzi wataweza kuhusisha kichocheo na yale wanayofahamu akilini. Vitabu vya kiada vinafaa kuwa vichocheo maalum vinavyoweza kuibua mwitikio chanya kwa ujifunzaji wa Kiswahili. Kuna hali tata hapa kwani walimu wa Kiswahili nchini Uganda wana ugumu wa kupata vitabu faafu na walivyo navyo ni vile vya asili ya Kenya ilhali silabasi yao ni tofauti na ya Kenya. Baadhi ya vitabu hivyo ni vya ngazi ya juu kuliko mahitaji ya wanafunzi wa Uganda kwa kuwa mafunzo ya Kiswahili nchini Uganda hayajakita mizizi. Kwa mwelekeo huo sifa za mabadiliko miongoni mwa wanafunzi, zitaweza kuibuliwa tu iwapo vitabu vitakavyotumika vitazingatia tajiriba ya Uganda, na vitalenga mifano na silabasi ya Kiswahili nchini Uganda. Vifaa vinavyotumika pamoja na mbinu za kufundishia zote zinapaswa kuzingatia kiwango cha lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

**Hitimisho**

Sura hii imeelezea umuhimu wa maandalizi ya walimu katika kukuza walimu faafu watakaofanikisha maendeleo ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Imenuia kubainisha pengo lililopo katika maandalizi ya walimu nchini Uganda hususan katika kaunti ya Bugiri. Maandalizi bora yatamjenga mwalimu mwenye mtazamo bora kuhusu somo la Kiswahili, haiba nzuri, anayetumia mbinu bora na vifaa mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili. Hadhi ya Kiswahili imeimarika, na idadi ya watu wanaozungumza Kiswahili duniani inazidi kukua kila uchao. Matumizi yake katika mawasiliano yanaunganisha jamii mbalimbali. Kiswahili ni chombo muhimu kwa shughuli za kitaifa na kimataifa. Nchi ya Uganda haina budi kukijenga Kiswahili ili kuwa sehemu ya mawasiliano ya kitaifa na kimataifa. Mikakati imewekwa ili kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kwa mujibu wa mkaguzi wa Elimu katika Kaunti ya Bugiri, serikali imeteua shule tatu ambazo kwazo inafanya majaribio ya ufundishaji wa Kiswahili ili ipate kuanzisha masomo rasmi ya Kiswahili katika nchi ya Uganda. Ili kufanikisha lengo hili, lazima serikali na walimu binafsi wazingatie kuboresha maandalizi ya walimu ili waweze kukabiliana na ufundishaji wa somo la Kiswahili nchini Uganda. Tunahoji kuwa kushindwa kwa hali ya Kiswahili nchini Uganda kiakademia na kimawasiliano hakuhusiani na

silabasi, bali kunahusiana na maandalizi chapwa ya walimu. Jinsi jamii inavyobadilika ndivyo inavyotarajiwa kuwa maandalizi ya walimu pia yafanyiwe marekebisho ili kuingiliana ipasavyo. Kuna haja ya walimu kuandaliwa vyema katika vyuo vikuu ili wawe tayari kukabiliana na changamoto zozote nyanjani.

Maandalizi wanayopewa walimu yanapaswa kukuza sifa ambazo zitajitokeza katika mitazamo chanya kuhusu somo la Kiswahili, haiba nzuri, mbinu na vifaa bora vya kutumiwa katika ufundishaji. Maandalizi ya walimu yanapaswa kutilia maanani vigezo mbalimbali ambavyo ni lazima vitekelezwe ili kuwepo na ufundishaji bora, asemavyo Gag'ne (1965).Vigezo hivi hapa ni mwalimu, mazingira ya ufundishaji, vifaa na mbinu za ufundishji. Hivyo basi,walimu wa Kiswahili wanapaswa kuwa na sifa nyeti za kihaiba ambazo zinafanya kusoma kuwe kwa maana zaidi na kwa kuvutia ili kuzidisha kuinua kwa lugha na kukomesha mwelekeo wa matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa na pia kushindwa kuwasiliana ipasavyo katika hali halisi nje ya darasa. Aidha, walimu wa Kiswahili nchini Uganda kama asemavyo Sifuna (1996), wanapaswa kuhudhuria warsha, makongamano na mikutano ili kupigwa msasa. Msaada huu utawafanya walimu kujenga uhusiano na kupata ufafanuzi kutoka kwa walimu wengine na wataalam ambao watashirikiana nao. Hili litaimarisha mitazamo ya walimu juu ya maudhui na mbinu zake za ufundishaji. Tunapendekeza kuwa mitazamo ya walimu wanaofunza Kiswahili nchini Uganda ipigwe msasa kwa kuhudhuria semina na warsha.

Mwalimu anafaa kuwa mbunifu ili kutia uhondo kwa masomo kwa vifaa vya kuvutia vya ufundishaji, kubadili mandhari ya darasa, kazi, na jinsi ya kukaa ili kufanya mazingira yavutie. Vilevile, watumie teknolojia kama vile utandawazi na vifaa tamba kama rununu ambavyo ni maarufu mno kwa wanafunzi. Haya yatafanya mtagusano wa mwalimu na wanafunzi kuwa bora. Taaluma ya Kiswahili nchini Uganda kama yalivyo masomo mengine inatarajiwa kuandaa na kufundisha kozi ambazo zinakubaliana na matarajio pamoja na mabadiliko katika jamii. Idara za Kiswahili kwa mfano ziwe tayari kujifahamisha na kujiandaaa kwa mabadiliko yoyote katika mitaala ya asasi za mafunzo hasa shule. Serikali na walimu wa Kiswahili nchini Uganda wanapaswa kuhakikisha kuwepo na kutumika kwa teknolojia kwa kununua vifaa kama runinga,redio,simu,tarakilishi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara shuleni ili kuhakikisha kuwa vinatumiwa. Ni muhimu kwa serikali kuteua vitabu faafu vya kutumiwa kwa kufundishia Kiswahili nchini Uganda. Pengo la ukosefu wa vitabu linaweza kupunguzwa kwa kuwateua waandishi wenye tajriba ili kuandaa vitabu mwafaka vinavyoendana na mtalaa. Mtalaa unapaswa kuwekwa kwa kila shule ili urejelewe na walimu. Mada katika mtalaa na vitabu vya kiada zipangwe kuanzia nyepesi hadi ngumu ili kuwamotisha walimu na wanafunzi. Vijelezi vitolewe kwa lugha nyepesi kueleweka kisha mada zielezwe kwa uwazi na undani na kutolewa mifano mwafaka. Mifano isawiri mazingira ya mwanafunzi ili ajitambulishe nayo. Mada zenye umuhimu kwa mwanafunzi ni rahisi kujifunza na kukumbuka. Ni muhimu mada kwenye vitabu vya kiada zitolewe muhtasari mwishoni mwa sura ili kurahisisha udurusu. Mazoezi ya kutosha na yanayolenga mada yanahitajika ili kumwezesha mwanafunzi kutumia kanuni alizounda katika ujifunzaji kutatua matatizo mapya. Kwa kweli maandalizi bora ya walimu yatachangia mmo katika kuimarisha ufundishaji wasomo la Kiswahili nchini Uganda.

## Marejeleo

Bandura, A. (1977). Self Efficacy: Toward a unifying theory of behavior change. *Psychological Review*, 84,191-215.

Barnes, R. E., & Aguarrrebere, J. A. (2006) Sidetracking the debate on teacher Quality. *Education Week*, 26(12).

Burudi, J. (2009). *Mtazamo wa walimu na wanafunzi kuhusu maudhui ya isimu katika silabasi ya Kiswahili shule za sekondari nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia.

Darling-Hammond, L,., & Berry, B. (2006). Highly qualified teachers for all. *Educational Leadership*. 64(3) 14-20.

Dornyei, Z. (2009). Communicative Language teaching in the 21st century: the principled Communicative approach. *Perspective* –Fall.Vol, **XXXVI** (2): 41-42.

Egessa, D. (2007). *Uhakiki wa matatizo yanayowakumba walimu katika utekelezaji wa silabasi za shule za upili, wilaya ya Kakamega, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolijia cha Masinde Muliro.

Gareett, M. A. (2009). *Teacher personality: does it influence effectiveness and a student achievement in the classroom?* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Rowan.

Hooper, D. W. (2002). Improving Instruction as a team. *School Adminstrator*, **59** (41): 42- 44. Katika: Kate Parry (Wah) Language and a Literacy in Uganda: Towards a Sustainable Reading Culture, pp. 1-5. Kampala: Foundation Publishers.

Kang'ahi, M. (2016) '*Influence of Pedagogical Styles on students Academic Achievement in Kiswahili in secondary Schools in Kakamega North Sub-County, Kenya*." Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Maseno.

Koteng', G. A. (2009). '*The influence of verbal communication interraction patterns on learners' participation in the classroom among secondary schools in Kisumu Town*." Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Moi.

Laczko- Kerr, I., & Berliner. D. (2003). In harm's way.*Educational Leadership*, 60(8),1-9.

Mukama, R. (1989). "Hali na Hadhi ya Kiswahili Nchini Uganda" Katika *Makala za Mkutano wa Kimataifa wa Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and Its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A Case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies*.

Muthwii, M. (2002). *Language Policy and Practices In Education In Kenya and Uganda*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Ndoleriire, O. (1996). "Kiswahili as a National Language: Towards Language Homogeneity or Heterogeneity, The Vexing National Language Issues in Uganda" Katika *Makerere Papers in Language and Linguistics, Journal of the Institute of Languages of Makerere University*; Vol. 1 No3 1996

Odeo, I. I. (2003) "*Oral questioning in the pedagogy of Kiswahili grammar: a study of teachers' practices in selected secondary schools of Bungoma district, Kenya*." Unpublished thesis. Moi University.

Porter-Margee, K. (2004)Teacher quality controversy and *NCLB*. *The Clearing House*, 78(1), 26-29.

Sifuna, D. (1989). *Development of Education in Africa: The Kenyan Experience*. Nairobi: Initiatives Publishers.

Walker, R. J. (2008) Twelve characteristics of an effective teacher.Longitudinal, qualitative quasi-research study of in-service teachers' opinions.*Educational Horizons*.61-68.